

TANGAZO LA SERIKALI NA. 367 la tarehe 4/9/2015

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA
(SURA 290)

SHERIA NDOGO

(Zimetungwa Chini ya Kifungu cha 6 (1) na 16(1))

SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA ASALI) ZA HALMASHAURI YA MANISPAA
TABORA, 2014

Jina 1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za
(Ushuru wa Asali) za Halmashauri ya Manispaa ya Tabora za
mwaka 2014 na zitaanza kutumika mara baada ya kutangazwa
katika Gazeti la Serikali.

Eneo la Matumizi 2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika maeneo yote yaliyo
chini ya mamlaka ya Halmashauri ya Manispaa ya Tabora.

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa kama
itakavyoelekezwa vinginevyo:-

“Afisa Mwidhinishwa” Maana yake ni Afisa wa Halmashauri
au Wakala alliyeidhinishwa na Mkurugenzi kusimamia
utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

“Halmashauri” Maana yake Halmashauri ya Manispaa ya
Tabora.

“Mfanyabiashara” Maana yake ni Mtu yeyote, Kampuni,
Shirika, Taasisi, Kiwanda chochote, ambaye au ambacho
kinafanya biashara ya kutengeneza, kuuza, kusafirisha au
kuhifadhi asali katika eneo la Halmashauri.

“Mkurugenzi” Maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Tabora ikiwa ni pamoja na Afisa yeyote wa Halmashauri anayekaimu wadhifa wa Mkurugenzi kwa wakati huo.

“Sheria” Maana yake ni sheria ya fedha za Serikali za Mitaa.

“Ushuru” Maana yake ni kiwango cha fedha kilichopangwa na Halmashauri kitakachotozwa dhidi ya mfanyabiashara wa asali.

4.-(i) Halmashauri itatoza ushuru wa asali kutoka kwa wafanyabiashara wa bidhaa hiyo waliopo katika eneo la Halmashauri kwa kiwango cha asilimia tano (5%) kwa kila galoni la lita tano ya asali hiyo, ama kiwango cha asilimia ishirini (20%) kwa kila ndoo ya lita ishirini ya asali hiyo.

(ii) Halmashauri itatoza ushuru wa Nta kwa wafanyabiashara wa bidhaa hiyo kwa kiwango cha shilingi mia tano (500/=) kwa kila kilo moja (kg I) ya Nta.

5. Ni marufuku kwa mtu yeyote kuuza, kusafirisha au kuhifadhi asali katika eneo la Halmashauri bila kibali cha Halmashauri.

6. Ili kupata kibali kwa mujibu wa kifungu 4(2) kama inavyotajwa hapo juu katika Sheria Ndogo hizi, mfanyabiashara atawajibika kulipa ushuru kwa Halmashauri kupitia Afisa Mwidhinishwa aliyeteuliwa kukusanya ushuru huo kwa niaba ya Halmashauri.

7. Halmashauri inaweza kumteua mtu binafsi, Kampuni, Asasi na Taasisi kukusanya ushuru wa asali kwa niaba yake.

8. Wakala aliyeteuliwa atakuwa na majukumu yafuatayo:-

- a) Kukusanya na kupokea ushuru kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alilopangiwa na kwa kiwango kilichoainishwa chini ya Sheria Ndogo hizi;
- b) Kuwasilisha makusanyo yote aliyowajibika kukusanya kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala aliongia na Halmashauri;
- c) Kumchukulia hatua za kisheria mtu yeyote ambaye atakiuka masharti ya Sheria Ndogo hizi.

9. Itakuwa ni kosa kwa wakala yeyote chini ya Sheria Ndogo hizi:-

- a) Kushindwa kuwasilisha fedha kwa kiwango kilichoainishwa katika mkataba bila sababu za msingi;
- b) Kukusanya kiwango zaidi ya kile anachostahili kukusanya.

10. Mtu yeyote, awe ni mfanyabiashara, mnunuzi au muuzaji au wakala ambaye:-

- i) Atakataa au kukwepa kulipa ushuru;
- ii) Atamshawishi mtu yeyote au kundi la watu wasilipe ushuru
- iii) Atamzuia Afisa muidhinishwa au Wakala kutekeleza majukumu yake

iv) Atadanganya na kuhusiana na kitendo chake hicho
ataikosesha Halmashauri mapato yake.

Atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini
isiyozidi shilingi elfu hamsini(50,000/=)au kifungo cha miezi
mitatu jela au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na
kifungo.